SCRIPTURE MWITO PROG 1083 KISWAHILI SCRIPT

ROMANS-: 5:6

TRANSWORLD RADIO

INTRO:

Nakukaribisha tena msikilizaji wangu kwa kipindi cha MWITO nambari 1082 kutoka studio zetu za Nairobi.Sina shaka kwamba Mungu amekulinda na hata kukufikisha siku ya leo ambapo tunakutana tena.Nakukumbusha kuwa kipindi hiki kinakujia kwa hisani na udhamini wa huduma ya kimataifa ya Macedonian Call yae Harod Williams

Kwa dakika 15 zijazo utafaidika kwa neno kutoka huduma ya mchungaji huyu.IKiwa ungependa upikea habari zaidi kuhusu huduma hii nitakupatia amwani mwishoi mw kipindi hiki.Naomba uweke Bibilia yao karibu ili kusikiliza kipindi hiki na ikiwa umemwalika mwenzako hiyo ni vyema sana.Tunendelea kusoma kutoka kitabu cha Warumi sura ya 5.Labda kwa wale ambao hamukuwa nasi nawakumbusha kuwa tulisoma aya za 1 hadi ya 2 ya sura hiyo.Nawakumbusha tu kwa muhtasari kwamba tutazisoma aya zote tano kisha tutaendelee-"***Basi tukishakuhesabiwa haki itokayo katika imani,na mwe na amani kwa Mungu,kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo,ambaye kwa yeye tumepata kwa njia ya amani kuifikia neema hii ambayo mnasimama ndani*** yake ***na kufurahi katika tumaini la utukufu wa Mungu."***…***Wala si hivyo tu,ila mfurahi katika dhiki pia; ….mkijua kuwa dhiki kazi yake ni kuleta saburi,na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo;na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini na tumaini halitahayarishi,kwa mana neno la Mungu limekwisha kumiminwa katika*** mioyo ***yetu na Roho mtakatifu***.

Na sasa ningependa tuongezee aya ya 6***….Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu,wakati ulipotimia Kristo alikufa kwa ajili ya waovu.Kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki;lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema.***

Naam bila shaka huu ni mstari au aya yenye nguvu.Inasema mengi kwa maneno machache.Tulipokuwa hatuna nguvu..Je? hii inamaanisha nini? Naam kulikuwa na wakati mmoja wakati tupokuwa tukiishi dhambini,ambapo hatukuwa na namna ya kujisaidia.Yaani dhambi ilituzingira na kutushika mateka.Tulikuwa watumwa wa dhambi.Dhambi ilikuwa mfalme katika maisha yetu.Hiyo ndivo dhambi inavyofanya.Inakolea maisha yako na kukudhoofisha.Hata hivyo ndani yetu kungalipo na kitu ambacho Mungu alituuumbia ndani kinachotaka uhusiano na

MUngu.Kinachotaka uhusiano huo urekebishwe.Mwenye dhambi anatawaliwa kiasi cha kutoweza kujikwamua kutoka kwenye inamasi au tope la mwovu shetani.

Daudi alikuwa na furaha na alifurahi jinsi tunavyosoma katika Zaburi 40 aliposema…"***Nalimgoja Bwana kwa saburi,akaniinamia akasikia kilio change,akanipandisha kutoka shimo la uharibifu,toka udongo wa utelezi,akaisimaisha miguu yangu mwambani,akaziimarisha hatua zangu.Akatia wimbo mpya kinywani mwangu.,ndio sifa zake Mungu wetu.Wengi wataona na kuogopa ,Nao watamtumini Bwana.Heri aliyemfanya BWANA kuwa tumaini lake,wala hakuwaelekea wemye kiburi.***

Mpendwa msikilizaji wangu Daudi alimaizi kuwa pekee yake katika hali yake ya dhambi hangeliweza kukabiliana na hali iliyomkumba.Ni Mungu tu ambaye angelimpandisha kutoka shimo la uharibifu,toka udongo wa utelezi na kuisimamisha mguu yake mwambani.Tujuavyo mtu katika hali kama hiyo hawezi kujiokoa na hutegemea usaidizi.Ndivyo tulivokuwa tulipokuwa tumelemewa dhambini.Lakini wakati ulipowadia.Wakati wa wa Mungu.Alimtuma mwanae Yesu Kristo kutokoa na kutukomboa dhambini.Huo wakati ulikuwa umepangwa na Mungu mwenyewe.Wakati wa ukombozi wa mwanadamu.Katika kitabu cha Wagalatia tunaambiwa kuhusu mambo kutendeka katika utimilifu wa wakati.ungu alimtuma mwanawe Yesu Kristo kutufia msalabani.Utimilifu wa kati ni wakati mteule ambao Mungu alionelea kwamba wafaa kumtuma mwanawe hapa duniani ili kuweka daraja kwa watakaomkubali maishani mwao waipitie ili kumrudia Mungu Baba.Huo ulikuwa wakati mwafaka kabisa wakati wa Mungu mwenyewe kutekeleza jukumu lake.Kusudi lake kumhusu binadamu.Upendo wa Mungu ulithibitishwa wakati huo kupitia mwanawe Yesu Kristo.Kumbuka manabii walitabiri kuzaliwa kwa mkombozi Yesu Kristo ,wakati na mahala penyewe .Hoi la kulia ngómbe mjini Bethlehemu.Ilitabiriwa kuwa Mesiya angezaliwa katika Bethlehemu ya Yuda.Wengi walitazamia na kutarajia mwana ambaye angezaliwa katika jamaa ya kifalme,katika jumba la kifahari ,lakini ukweli wake ulitokea kuwa kinyume.

Naam utimilifu wa wakati hauji mapema wala hauchelewi.Naam Kristo alikufa kwa ajili ya mwanadamu mwenye dhambi..yeye ambaye hakuwa na dhambi.Alijitwika dhambi zetu kwenye msalaba pale kalvari.Aya ya saba inasema ya kitabu cha Warumi sura ya 7 inasema….***kwa kuwa ni shida mtu kufa kwa ajili ya mtu mwenye haki;lakini yawezekana mtu kuthubutu kufa kwa ajili ya mtu aliye mwema.***

Ningepeda tukomee hapa kwa leo.Tutaendelea kwenye kipindi kijacho kufafanua kuhusu usemi huo.Namalizia kwa kukuuliza wewe mwenzangu swali moja ,tena jepesi mno.Wewe ulikuwa mtu mzuri,au mtu mzuri alikufa kwa ajili

yako? Je? Umempokea Yesu kuwa mwokozi wa maisha yako? Ikiwa bado hii ni fursa nzuri ya kufanya hivyo.Jinsi mfano tuliopewa katika kitabu cha Mwanzo sura ya 22,wakati Ibrahimu alikuwa tayari kumchinja mwanawe Isaka.Mungu alishika mkono wake ungali juu na kumwambia usimchinje mwanao Ibrahimu ,tazama mwanakoncdoo.Nakumbuka kwaya moja iliimba wimbo mzuri sana kuhusu tendo hilo la imani kuu.Kondoo alitolewa kuwa sadaka mbadala ya kuteketeza.Asingelikuwa Yule kondoo,Isaka angelichinjwa na uzao ambamo alizaliwa Yesu mwokozi wetu ungeliangamizwa.

Naam mpendwa ninapokamilisha kipindi hiki ,sijui ikiwa ushakubali kumpokea Kristo awe mwokozi wako.Labda umekuwa ukimtoroka kwa siku au miaa mingi.Utachukua hatua leo? Utamfungulia mlango wa moyo wako ili apate kuingia?Ikiwa jibu lako ni ndio ningependa utubu dhambi zako leo na kumpokea rohoni mwako ili akue dira mpya maishani mwako.Usije ukatahayari siku ya mwisho,wakati wateule wake watakapopanga foleni kuingia Jerusalemu mpya.Mbinguni ambako tumeandaliwa makao.Chukua hatua hiyo sasa hivi.

Hiki kimekuwa kipindi cha Mwito nambari 1083.Naomba uwasiliane nami kupitia njia ya arafa ukitumia nambari ifwatayo-: 0721 970 520. Au 020 2679842.Ikiwa unaishi Nairobi tunakukaribisha ututembelee kwenye studio zetu za TWR Kamburu Drive,off Ngong Road, baada ya jumba la TOP PLAZA.Anwani yangu ikiwa utaniandikia barua ni-:Kwa mtayarishi,Mwito,S.L.P.21514-00505 Nairobi.Waweza pia kuwasiliana nami kwa njia ya barua pepe ifwatavyo-barua@twr.co.ke.Na basi kufikia hapo sina budi kulikunja jamvi langu kwa leo ninapokutakia baraka sufufu kutoka kwake Mungu wetu mtukuka.Juma lijalo tutaingia aya ya 7 ya sura ya 5 ya kitabu cha Warumi.Ni mwaandazi wa kipindi hiki ndugu Charles Otunga ninayekuaga nikikutakia mbawazi zake Mungu wetu mtukuka.Kwaheri.

Xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx